Jinsi Kirangi Kinavyoandikwa

Alfabeti ya Kirangi

a b ch d e f g h i ɨ j k l
m n ng' ny n'y o p r s sh
t u ʉ v w y yy

Jinsi Kirangi Kinavyoandikwa

Huduma ya Kuendeleza Lugha za Asili
Mkoa wa Dodoma
S.L.P. 1369
Dodoma, Tanzania

Kichwa: Jinsi Kirangi Kinvyoandikwa

Lugha: Kirangi / Kiswahili

Kimetengenezwa na: Lizzie Poole

Pamoja na timu ya Warangi: Paulo Kijuu, Emelia Issaka

Picha: Global Partners images with permission. © SIL International 2009. Images used with permission. Creative Commons BY-SA 4.0

© 2024 SIL International

Herufi za Kirangi zinazofanana na zile za Kiswahili

Herufi hizi hazitakuwa ngumu kwako kujifunza. Ni zile zile katika Kirangi na Kiswahili. Sasa tufanye mazoezi ya kusoma herufi zifuatazo.

Irabu: **a, e, i, o, u**

Konsonanti: **b, ch, d, f, g, h, j, k, l, m, n, ng', ny, p, r, s, sh, t, v, w, y**



mburi
(mbuzi)



ng'onyu
(funza)



ichimu
(mkuki)



irino
(uyoga)



inkwi
(kuni)



njoka
(nyoka)

ludihi
(kamba)

mawye
(mawe)

vasinga
(watoto)

Kama tulivyoona, herufi nyingi za Kirangi zinafanana na herufi za Kiswahili. Lakini, kuna vitu vichache tofauti ambavyo tumeona vizuri tuvieleze hapa ili watu watakaosoma kwa mara ya kwanza, waweze kusoma Kirangi vizuri. Vitu hivi ni:

(A) Konsonanti mpya: **n'y** na **yy**

(B) Irabu za katikati: **ɨ** na **ʉ**

(C) Irabu ndefu

(D) Tuni au muziki

(A) Konsonanti mpya: n'y na yy

Herufi **ny** ipo katika Kiswahili na Kirangi, lakini pia Kirangi kina herufi **n'y**. Zingatia kutofautisha herufi ya **ny** na herufi ya **n'y**. Herufi ya **ny** inawakilisha sauti moja tu kama katika Kiswahili, lakini **n'y** inawakilisha sauti mbili, yaani **n** ikifuatwa na **y**. Linganisha maneno haya:

ny	**n'y**
ka**ny**a *(angusha)*	kaa**n'y**a *(kataza)*
kiri**ny**a *(nyamaza)*	yere**n'y**a *(linganisha)*

Pia, kwa Kirangi kuna **yy**, pamoja na **y**. Zingatia kutofautisha herufi ya **y** na herufi ya **yy**. Herufi ya **y** inasikika kama sauti moja tu, lakini **yy** inasikika kama herufi mbili. Linganisha maneno haya:

y	**yy**
lʉjo**y**a *(unyoya)*	o**yy**a *(osha)*
ubu**y**a *(ulafi)*	ntu**yy**a *(twiga)*

(B) Irabu za katikati: ɨ na ʉ

Kiswahili kina irabu tano tu, ambazo ni a, e, i, o, u. Lakini Kirangi kina irabu saba: **a, e, i, ɨ, o, u, ʉ**. Herufi za **ɨ** na **ʉ** zinaitwa irabu za katikati kwa sababu **ɨ** inatamkwa katikati ya e na i, na **ʉ** inatamkwa katikati ya o na u. Angalia mifano inayofuata ili kujua umuhimu wa kuandika irabu hizi, na kujifunza sauti zake:

Irabu kama Kiswahili (i, u)	**Irabu za katikati (ɨ, ʉ)**
r**i**ma *(zima)*	r**ɨ**ma *(lima)*
imbw**i** *(mvi)*	**ɨ**mbw**ɨ** *(buibui)*
ny**i**ng**i**r**i** *(chawa)*	ng**ɨ**r**ɨ** *(ngiri)*
ichim**u** *(mkuki)*	irim**ʉ** *(baragumu)*
ng**u**r**u**r**u** *(nguvu)*	ng**ʉ**r**ʉ**ve *(nguruwe)*
m**u**viri *(sehemu iliyolimwa)*	m**ʉ**vɨrɨ *(mwili)*

(C) Irabu ndefu

Kirangi kina irabu ndefu, yaani, zinatamkwa kama zinavutwa kwa muda. Irabu ndefu huandikwa na herufi mbili pamoja, kwa mfano:

Irabu fupi	**Irabu ndefu**
kʉt**a**ha *(kuchota)*	kʉt**aa**ha *(kuzika)*
k**e**nde *(karibu ya)*	k**ee**nde *(tangu)*
if**i**ya *(figa)*	f**ii**ya *(fyonza)*
k**ʉ**la *(kua)*	k**ʉʉ**la *(chomoa)*

Mara chache, irabu zilizo sawasawa ziko pamoja lakini zisitamkwe kama irabu ndefu. Inasikika kama kuna pumziko katikati. Pumziko hili liandikwe kwa kutumia alama ya mkato mahali sauti inapobadilika. Angalia mifano inayofuata:

Miiririkano yaanyu ɨve **ɨ'ɨra** Kirisitʉ Yéesu ^ajáa noyo.	*Mawazo yenu yawe **yaleyale** Kristo Yesu alikuwa nayo.*
Mweenevyoosi nɨ yeeye **ʉ'ʉra** ʉmwɨ.	*Mwenyevyote ni yeye **yuleyule** mmoja.*
Miiro ya Mʉlʉʉngʉ yaanjéryaa mʉtɨma **isi'iisii** mutimii waanɨ.	*Sheria ya Mungu hunifurahisha roho **ndani kabisa** moyoni mwangu.*

(D) Tuni au muziki

Kwa Kirangi tuni, au muziki, ya maneno hutofautisha maana. Kwa mfano, neno **isaare** inawezekana kuwa na maana ya *neno*, au *mchanga*. Maana yake inategemea na jinsi inavyotamkwa. Alama ya kupandisha sauti inamsaidia msomaji atamke vizuri anaposoma. Irabu yenye alama, kwa mfano **á**, inatamkwa na sauti ya juu. Angalia mifano inayofuata:

Irabu	**Sauti ya juu**	**Sauti ya chini**
a	ibáta *(bata)*	mbava *(mabawa)*
ɨ	nchɨ́lɨ *(mende)*	ngɨrɨ *(ngiri)*
o	nkóru *(kovu)*	nkome *(fimbo)*
u	nkúru *(kobe)*	nkuru *(kipeyu)*

Irabu ndefu inawezekana kutamkwa juu (***áá***) au chini (***aa***) lakini pia inawezekana kutamkwa na sauti inayoshuka (***áa***), au sauti inayopanda (***aá***). Angalia mifano inayofuata:

Irabu	**Sauti ya juu**	**Sauti ya chini**	**Sauti inayoshuka**	**Sauti inayopanda**
aa	mp**áá**ha *(ukucha)*	mp**aa**nga *(pango)*	is**áa**re *(neno)*	is**aá**re *(mchanga)*
ee	lʉv**éé**ngʉ *(kongosho)*	lʉh**ee**mbe *(pembe)*	mp**ée**sa *(pesa)*	ip**eé**ne *(nyonga)*
ii	ir**íí**mba *(banzi la mlango)*	mw**ii**wi *(mshale)*	ir**íi**mba *(zeze)*	mw**ií**wi *(mbuyu)*
ɨɨ	mbɨr**ɨ́ɨ́**ra *(kaburi)*	mʉlw**ɨɨ**rɨ *(mpiganaji)*	mʉlw**ɨ́ɨ**rɨ *(mgonjwa)*	
oo	mp**óó**ngo *(hadithi)*	ik**oo**chi *(mdudu)*	ik**óo**chi *(kochi)*	ik**oó**nchi *(kiguru)*
uu	muk**úú**nku *(makapi)*	ik**uu**ta *(aina ya panya)*	nk**úu**mba *(tai)*	ik**uú**ti *(goli)*
ʉʉ	mʉk**ʉ́ʉ́**lʉ *(mkuu)*	kɨk**ʉʉ**ngʉ *(aina ya maradhi)*	kɨk**ʉ́ʉ**ngʉ *(kikwaru cha jogoo)*	ik**ʉʉ́**ngʉlʉ *(kunguru)*

Pia, alama ya kupandisha sauti inatumika kwa kutofautisha wakati wa matendo. Tukiandika **nabokaa** haiko wazi kama maana ni *mimi huchimba*, au *nilikuwa huchimba*. Ndiyo sababu ya kuandika alama ya kupandisha sauti.

Katika nyakati zilizopita, tunaandika alama ya kupandisha sauti juu ya irabu ya silabi ya mwisho ya neno. Kama silabi ya mwisho ina irabu ndefu, tunaandika alama juu ya irabu yake ya kwanza. Katika nyakati za sasa tunaandika alama ya kupandisha sauti juu ya irabu ya kwanza ya mzizi. Mzizi wa neno ni sehemu inayobeba maana, kwa mfano *boka, doma, chereva*. Angalia mifano:

Wakati uliopo (alama kwenye mzizi)	**Wakati uliopita** (alama kwenye silabi ya mwisho)
nab**ó**kaa *(mimi huchimba)*	nabok**áa** *(nilikuwa huchimba)*
ad**ó**maa *(yeye huenda)*	adom**áa** *(alikuwa huenda)*
ad**ó**mire *(ameenda)*	adomir**é** *(alienda jana)*
mʉch**é**revire *(mmechelewa)*	mʉcherevir**é** *(mlichelewa jana)*

Kuna alama moja nyingine inayosaidia msomaji asome vizuri. Alama hii inaitwa alama ya kishazi rejeshi, na ni hiyo: **ˆ**. Kishazi rejeshi kinarejea kitu kingine na kinatoa taarifa zaidi juu ya kitu hicho. Kwa mfano, tuone sentensi za Kiswahili:

(1) Watu wakiume wote **waliokula siku hiyo** walikuwa elfu tano.

Maneno **waliokula siku hiyo** ni kishazi rejeshi kwa sababu yanarejea watu wakiume, na yanatoa taarifa zaidi juu ya watu hao. Yanatuletea taarifa kwamba wao walikula siku hiyo. Kwa Kiswahili vishazi rejeshi ni wazi kwa sababu vitenzi vina herufi zaidi. Linganisha *walikula*, na *wali**o**kula*. Au, mara nyingine kuna neno kama *ambaye, ambao* nk. Kwa hiyo, kwa Kiswahili tunaweza kuandika:

(2) Watu wakiume wote **ambao walikula siku hiyo** walikuwa elfu tano.

Maana ya sentensi (2) ni sawasawa na sentensi (1).

Kwa Kirangi tuni, au muziki, hutumika kuonyesha kishazi rejeshi. Kwa kuandika, tofauti ni wazi tukiandika alama ya kishazi rejeshi. Sentensi (1) iandikwe kwa Kirangi hivyo:

(3) Vaantʉ valʉme voosi **ˆvaarya** sikʉ ɨyo nɨ mayana yasaano.

Msomaji anajua kwamba sentensi itaendelea na atajua kutamka vizuri. Bila alama hiyo, msomaji atafikiri kwamba sentensi inamaliza hivyo:

(4) Vaantʉ valʉme voosi vaarya sikʉ ɨyo.

na atapata shida atakapogundua kwamba kuna maneno mengine, **nɨ mayana yasaano**, yanayofuata.

Kama kuna neno kama **mweene**, **reene**, **vyeene** (kwa Kiswahili *ambaye, ambalo, ambavyo* nk) tunaandika alama ya kishazi rejeshi nyuma ya neno hilo. Kama hakuna neno kama hayo, tunaandika alama nyuma ya kitenzi. Angalia mifano:

Mʉʉntʉ mʉlʉme ˆ**mweene** awʉla iwʉnda yoosaaka rɨma mahalaga.	*Mwanaume ambaye alinunua shamba anataka kulima maharage.*
Muhíínja ˆ**yooyeenda** balibali yoorɨra.	*Msichana anayetembea barabarani analia.*
Kʉmʉkwaata ndɨrɨ mwiívi ˆ**ajáa aanjɨvɨra** mpia.	*Nitamkamata mwizi aliyeniibia pesa.*

Pia vishazi rejeshi vinaweza kutoa taarifa juu ya wakati matendo yanapofanyika, mahali matendo yanapofanyika, au jinsi matendo yanavyofanyika. Kiswahili kinatumia *-po-* na *-vyo-* ndani ya kitenzi kuonyesha maana hii. Kwa Kirangi maana inaonyeshwa na muziki tu. Hivyo, pia tunaandika alama ya kishazi rejeshi katika mifano hii, jinsi inavyoonekana hapo chini:

ˆ**Akateere** masáare ayo, akahwaalala.	*Aliposikia maneno haya, akashangaa.*
Vakʉʉja na kʉʉntʉ ˆ**ajáa**.	*Wakaja mahali alipokuwa.*
Abweeyya ˆ**vyeene** ajáa awyɨɨrwa.	*Alifanya jinsi alivyoambiwa.*

Lusímo lwa Musúngaati na Lasáaro

(Lʉ́ka 16:19-31)

Haaha, kʉjáa kwatɨɨte musúngaati ʉmwɨ, ^iivɨkɨráa ɨngo ja kɨtáani ^jiri gyaa ja kisúngaati, ^jalʉkwa na mputi ja kɨkomi. Na sikʉ joosi yeeye arijáa chóorya cha kibuya. Kei, kʉjáa kwatɨɨte mʉkɨva ʉmwɨ ^asewáa Lasáaro. Areetwáa, maa akavɨɨkwa mʉryaangwii kwaachwe. Ʉhʉ ajáa atɨɨte viloonda mʉvɨrɨ vʉʉ. Yeeye iikaláa mʉryaangwii na ajáa atɨɨte mpɨɨma yo rya mang'enyeng'enye ^yawíire ɨsɨ ya méesa kwa ʉhʉ musúngaati. Kei, kúri jʉʉjáa noo mʉnaampa viloonda vyaachwe.

Sikʉ ^jikalooke, ʉra mʉkɨva akakwya. Mirimʉ miija ɨkʉʉja noo mʉsʉmʉla, ɨkamʉtwaala fʉʉrʉ kɨpeembii cha Aburaháamu. Ʉra musúngaati ne akɨjoowulala na akataahwa. Yeeye akatamanya na ntarii. Ʉko uturikirii, akiinurirya miiso yaachwe na mweeri, maa akamoona Aburaháamu kwa kʉlɨ arɨ na Lasáaro. Aho, ʉra musúngaati

akamwaanɨrɨra Aburaháamu, 'Taáta Aburaháamu, naanga na riiso ra wʉʉja. Nooloomba ʉmʉtʉme Lasáaro atukye imaamba raachwe luujii, maa atoonyerye lurimii lwaanɨ sa lʉhole. Kɨkomi nɨ tʉrɨkɨra niise mʉnʉmʉʉnʉ mootwii ʉhʉ.'

Aho, Aburaháamu akamʉsea, 'Mwanawaanɨ, kʉmbʉkɨra, weewe mpɨɨndɨ ^ʉjáa mooyo, ʉjáa ʉtɨɨte viintʉ vyoosi ^vyabooha ^ʉsaakáa. Maa kaa, Lasáaro nɨ uturikiri vii apatáa. Haaha yeeye atúuriiwe mʉtɨma aha na weewe ʉmwaarɨ wootʉrɨkɨra mʉnʉmʉʉnʉ. Sɨ jeyyo vii tʉkʉ, katɨkatɨ yiiswi na nyuunyu kwatɨɨte iduundu ikʉʉlʉ mʉnʉmʉʉnʉ. Iduundu ɨro, ravɨɨkwa sa vaantʉ va kʉnʉ ^varɨ saaka kʉʉja nooko kwaanyu, vasiindwe fɨrɨra na vaantʉ va ʉko vasiindwe kʉʉja na kʉnʉ.'

Aho, ʉra musúngaati akasea, 'Haaha nookʉloomba ee taáta ʉmʉtʉme Lasáaro atamanye na kaayii kwa taáta wiitʉ. Ʉko natɨɨte vaaniitʉ vasaano. Lasáaro akavalʉme kutu sa karɨ luu vʉʉje na kʉnʉ kʉʉntʉ kwa uturikiri tʉkʉ.'

Maa kaa, Aburaháamu akamʉsea, 'Vaanaanyu vatɨɨte ʉtali wa Mʉ́sa na valáali na mʉtwe va Ijʉva, vayateere ayo!'

Ʉra musúngaati akamʉsea, 'Taáta Aburaháamu tʉkʉ! Koonɨ mʉʉntʉ afúfukire na adome akavawyɨɨre, aho, valandʉka varɨ fuma uvii waavo.' Aburaháamu akamʉsea, 'Koonɨ sɨ vatéerɨɨre yara ^yaandɨkwa nɨ Mʉ́sa na valáali na mʉtwe, sɨ varɨ ruma baa ya mʉʉntʉ afúfukire tʉkʉ.'